

CAMBRIDGE INTERNATIONAL EXAMINATIONS
General Certificate of Education Ordinary Level

SWAHILI

3162/01

May/June 2003

2 hours 30 minutes

Additional Materials: Answer Booklet/Paper

READ THESE INSTRUCTIONS FIRST

If you have been given an Answer Booklet, follow the instructions on the front cover of the Booklet.
Write your Centre number, candidate number and name on all the work you hand in.
Write in dark blue or black pen on both sides of the paper.
Do not use staples, paper clips, highlighters, glue or correction fluid.

Answer **all** questions.

At the end of the examination, fasten all your work securely together.

The number of marks is given in brackets [] at the end of each question or part question.

This document consists of **3** printed pages and **1** blank pages.



1 Translate into **English**:

- (a) Nilikuwa nipo kwenye basi nikitoka Malindi nilipokwenda kumtazama babu yangu. Alikuwa mgonjwa. Nilikaa huko siku sita. Alipoanza kupata nafuu, na kuweza kutembeatembea kidogo ndipo nilipoaga na kupata ruhusa ya kuondoka. Sasa nilikuwa narudi Nairobi. Nilikaa kimya nikisikiliza nyimbo za kaseti zikipigwa na dereva, huku nikitazama nje ya dirisha. Safari ilikuwa inakwenda vizuri. Saa zikapita.

Tulikuwa tunakaribia Nairobi. Basi lilikuwa linakwenda kwa kasi sana tulipokaribia daraja. Hapo lilikuwapo basi jingine likingoja kuvuka. Dereva wetu akajaribu kupunguza mwendo ili asimame nyuma yake, lakini breki zake hazikufanya kazi. Watu waliokuwa wamekaa mbele walianza kupiga makelele. Punde si punde, watu wote wakawa wanapiga mayowe, wakimuomba Mungu awanusuru.

Mabasi mawili yakagongana kwa kishindo kikubwa sana. Basi letu likapinduka, likalala ubavu. Sote tulitupwa. Mimi niliushika kwa nguvu mkono wa chuma wa kiti cha mbele. Ingawa chuma cha kiti hicho kilinipiga ubavuni, sikuumia sana. Kigae kilinikata kidogo usoni, na mguu wangu wa kulia uliumia kwa kupigwa na mzigo mzito wa abiria. [20]

- (b) Waajiri nchini wanatakiwa watoe nafasi za kazi kwa viziwi wenye sifa na elimu ya kuridhisha. Hivyo, fursa za viziwi kupata kazi zitakuwa sawa na zile za watu wasiokuwa na ulemavu huo. Mwito huu ulitolewa na Mjumbe wa Chama cha Walemavu. Mjumbe huyo alisema kwamba kukosa mawasiliano limekuwa tatizo kubwa miongoni mwa viziwi, au, viziwi na waajiri. Matokeo ni kwamba viziwi wanakosa nafasi za ajira hata kama wana elimu ya kutosha ya kuajiriwa.

'Viziwi hawakubaliki kwa kazi yoyote au wanapuuzwa kwa sababu tu ni viziwi,' alisema mjumbe huyo. Aliendelea kulalamika kwamba kuna shule saba tu za viziwi katika taifa zima. Shule hizo ni muhimu sana kwa viziwi kwa vile zinafundisha lugha ya alama na namna ya kuwasiliana. Upungufu wa shule hizo inasababisha viziwi wengi kutojua lugha ya alama. Hivyo, mawasiliano miongoni mwa viziwi linakuwa tatizo.

Shule zote zilizopo ni za msingi. Mjumbe alishauri kwamba lugha ya alama itumike katika ngazi zote za elimu. [25]

2 Translate into Swahili:

Many youths flock to big cities from villages in the expectation of leading lives of luxury and comfort. This is because they had not been given proper information regarding life in the cities, for their friends had sent them excellent reports of what a good time they were having there! These 'friends' were not telling them the truth. In reality, because of high unemployment in the cities, it is very difficult to get good jobs quickly. Youths from the villages could wait for months before getting jobs that give them just enough money to buy food and pay rent. And getting good accommodation is also a problem.

Let us take the example of the city of Dar es Salaam. Today, approximately three and a half million people live in that city. This is equivalent to ten percent of the total population of Tanzania. The population of Dar es Salaam has been increasing year by year since 1948 when the city only had 67,227 inhabitants. The problem of overpopulated cities is not unique to Tanzania. In fact, it is estimated that within the next thirty years, more than half the population of developing countries will be living in cities. [30]

3 Write about 120 words in Swahili on one of the following subjects:

- (a) The job I like doing best.
- (b) The protection of our environment.
- (c) The importance of water.

[25]

